JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

# SERA YA MAMBO YA NJE 2001

## (TOLEO LA MWAKA 2024)

MEI 2025

# DIBAJI

Kwa mujibu wa Tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu majukumu ya Mawaziri (Hati Idhini) kupitia Tangazo la Serikali Na. 619B la tarehe 30 Agosti 2023, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepewa jukumu la kulinda, kukuza na kuendeleza maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia uhusiano wake na nchi nyingine na jamii ya kimataifa.

Katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) inaongozwa na misingi ya kutoingiliwa mamlaka yake, mipaka ya nchi na uhuru wa kisiasa; kutetea uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia; kuendeleza ujirani mwema na kukuza umoja wa Afrika.

Vilevile, ni dhima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendeleza ushirikiano wa kiuchumi na washirika wa maendeleo; kuunga mkono sera ya kutofungamana na upande wowote; kuendeleza ushirikiano wa maendeleo baina ya nchi zinazoendelea; kushirikiana na Umoja wa Mataifa katika jitihada za kuleta maendeleo ya kiuchumi, amani na usalama; pamoja na kulinda mila na tamaduni za watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sera ya Mambo ya Nje inajielekeza katika maeneo kumi (10) ambayo ni: diplomasia ya uchumi; kukuza amani, usalama na utulivu wa kisiasa; kuratibu usimamizi wa mikataba na itifaki za kimataifa; ushiriki wenye tija katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na kutafuta rasilimali za kimataifa kwa maendeleo ya Taifa.

Maeneo mengine ya kipaumbele ni ushiriki na ushirikishwaji wa diaspora kwa maendeleo ya Taifa; kutumia kikamilifu fursa zinazotokana na uchumi wa buluu na kulinda na kutetea haki

za binadamu na utawala bora kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuzingatia mila,desturi na tamaduni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Sera inazingatia masuala mtambuka ambayo ni mazingira na mabadiliko ya tabianchi na usawa wa jinsia na fursa kwa vijana. Hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kujumuisha masuala ya usawa wa jinsia na fursa kwa vijana katika uhusiano wa kimataifa.

Maandalizi ya Sera hii yamezingatia miongozo mbalimbali ya kimataifa (mikataba, makubaliano na itifaki) ikiwemo Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika: Afrika Tuitakayo; Ajenda ya 2030 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu na Ajenda ya Addis Ababa ya Ugharamiaji wa Maendeleo. Maandalizi yake pia yamezingatia miongozo ya ndani ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050; mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu pamoja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Ili kuendana na mabadiliko ya dunia, Sera hii itafanyiwa mapitio pale itakapohitajika.

Aidha, maandalizi ya Sera hii yamejumuisha tathmini ya mkakati wa utekelezaji, na ukusanyaji wa maoni ambao ulikuwa shirikishi. Shukrani za dhati ziwaendee wadau wote walioshiriki kwa juhudi zao za pamoja na mchango wao katika maandalizi ya Sera hii. Mwisho, ili kufikia malengo yake, utekelezaji wa Sera hii utategemea kuungwa mkono na ushiriki wa wadau katika utekelezaji wake.

*Balozi* Mahmoud Thabit Kombo (Mb)
**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

# YALIYOMO


DIBAJI.......................................................................................i

YALIYOMO...................................................................................iii

VIFUPISHO.................................................................................vii

UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU.......................................x

**SURA YA KWANZA.................................................................1**

UTANGULIZI..............................................................................1

1.1. Usuli.....................................................................................2

1.2.1. Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya 2001.......................................................................................4

1.2.2. Kuimarika kwa Uhusiano wa Uwili.....................................5

1.2.3. Kuimarika kwa Mtangamano wa Kikanda..........................5

1.2.4. Kuimarika kwa Ushirikiano wa Kimataifa..........................8

1.2.5. Kuchochea Diplomasia ya Uchumi.....................................9

1.3. Changamoto Katika Utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje (2001)...............................................................10

1.3.1. Kuendelea kuwepo kwa Uhalifu wa Kuvuka Mipaka.....10

1.3.2. Kukosekana kwa Utulivu wa Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa..................................................................................12

1.3.3. Kutoridhiwa kwa Mikataba Iliyotiwa saini na Itifaki......13

1.3.4. Mwingiliano wa Uanachama Katika Jumuiya za Kikanda na Taasisi za Kimataifa..........................................................14

1.3.5. Matumizi Hafifu ya Kiswahili katika Diplomasia............15
1.3.6. Changamoto katika Uratibu wa Utekelezaji......................16
1.3.7. Mapungufu Katika Utafutaji wa Rasilimali......................17
1.4. Masuala Mapya ya Kisera....................................................19
1.4.1. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi............................19
1.4.2. Ushirikishwaji na Ushiriki wa Diaspora............................20
1.4.3. Msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi............................21
1.4.4. Haki za Binadamu na Utawala Bora.................................22
1.4.5. Jinsia na Vijana...............................................................24
**SURA YA PILI.........................................................................25**
MSINGI, DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA..................25
2.1. Msingi.................................................................................26
2.2. Dira, Dhima na Malengo.....................................................27
2.2.1. Dira....................................................................................27
2.2.2. Dhima.................................................................................27
2.2.3. Lengo Kuu..........................................................................27
2.2.4. Malengo Mahsusi...............................................................27
2.3. Misingi ya Sera ya Mambo ya Nje........................................28
**SURA YA TATU.......................................................................30**
MASUALA, MALENGO NA MATAMKO YA SERA.................30
3.0. Sera......................................................................................31
3.1. Diplomasia ya Uchumi.........................................................31

3.1.1. Lengo la Sera.....32
3.1.2. Matamko ya Sera.....32
3.2. Amani, Usalama na Utulivu wa Kisiasa.....32
3.2.1. Lengo la Sera.....33
3.2.2. Matamko ya Sera.....33
3.3. Mikataba, Makubaliano, Maazimio na Itifaki.....33
3.3.1. Lengo la Sera.....34
3.3.2. Matamko ya Sera.....34
3.4. Ushirikiano wa Uwili.....35
3.4.1. Lengo la Sera.....35
3.4.2. Matamko ya Sera.....35
3.5. Mtangamano wa Kikanda.....36
3.5.1. Lengo la Sera.....37
3.5.2. Matamko ya Sera.....37
3.6. Ushirikiano wa Kimataifa.....37
3.6.1. Lengo la Sera.....38
3.6.2. Matamko ya Sera.....38
3.7. Kiswahili Kama Nyenzo ya Diplomasia.....39
3.7.1. Lengo la Sera.....40
3.7.2. Matamko ya Sera.....40
3.8. Utafutaji wa Rasilimali.....40
3.8.1. Lengo la Sera.....41
3.8.2. Matamko ya Sera.....41
3.9. Uchumi wa Buluu.....42

3.9.1. Lengo la Sera....43
3.9.2. Matamko ya Sera....43
3.10. Ushirikishwaji na Ushiriki wa Diaspora....43
3.10.1. Lengo la Sera....44
3.10.2. Matamko ya Sera....44
3.11. Haki za Binadamu na Utawala Bora....45
3.11.1. Lengo la Sera....46
3.11.2. Matamko ya Sera....46
3.12. Masuala Mtambuka....46
3.12.1. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi....46
3.12.1.1. Lengo la Sera....47
3.12.1.2. Matamko ya Sera....48
3.12.2. Jinsia na Vijana....48
3.12.2.1. Lengo la Sera....48
3.12.2.2. Tamko la Sera....48

**SURA YA NNE....49**

MUUNDO WA KISHERIA....49
4.0 Muundo wa Kisheria....50

**SURA YA TANO....51**

MUUNDO WA KITAASISI....51
5.0. Muundo wa Kitaasisi....52
5.1. Ufuatiliaji na Tathmini....54
5.2. Hitimisho....55

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AfCFTA** | African Continental Free Trade Area |
| **AGOA** | African Growth and Opportunity Act |
| **AU** | African Union |
| **CBOs** | Community Based Organisations |
| **CCIAM** | Climate Change Impacts, Adaptation and Mitigation |
| **CHRAGG** | Commission for Human Rights and Good Governance |
| **COE** | Contingent- Owned Equipment |
| **CSOs** | Civil Society Organizations |
| **DCEA** | Drugs Control and Enforcement Authority |
| **DICOTA** | Diaspora Council of Tanzania in America |
| **DRC** | Democratic Republic of the Congo |
| **DTA** | Double Taxation Agreement |
| **EAC** | East African Community |
| **EBA** | Everything but Arms |
| **EEZ** | Exclusive Economic Zone |
| **EU** | European Union |
| **FDIs** | Foreign Direct Investments |
| **FIU** | Financial Intelligence Unit |
| **HRC** | Human Rights Commission |
| **ICCPR** | International Covenant on Civil and Political Rights |
| **ICTR** | International Criminal Tribunal for Rwanda |
| **INFF** | Integrated National Financing Framework |
| **IORA** | Indian Ocean Rim Association |
| **JCC** | Joint Committee for Cooperation |

| | |
|---|---|
| **JPC** | Joint Permanent Commission |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **MDAs** | Ministries, Departments and Agencies |
| **MINUSCAR** | United Nations Multidimensional Integrated Stabilization Mission in the Central African Republic |
| **MONUSCO** | United Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo |
| **MoU** | Memorandum of Understanding |
| **NCTC** | National Counter Terrorism Centre |
| **NFP** | New Foreign Policy |
| **NPS** | National Prosecutions Services |
| **NGOs** | Non-Governmental Organizations |
| **PCCB** | Prevention and Combating of Corruption Bureau |
| **PO – RALG** | President's Office, Regional Administration and Local Government |
| **RECs** | Regional Economic Communities |
| **RGoZ** | Revolutionary Government of Zanzibar |
| **RSs** | Regional Secretariats |
| **SALW** | Small Arms and Light Weapons |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SAMIM** | Southern African Development Community Mission in Mozambique |
| **SADC-RPTC** | Southern African Development Community Regional Peacekeeping Training Centre |
| **SADC – RCTC** | Southern African Development Community Regional Counter-Terrorism Centre |

| | |
|---|---|
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **TCCIA** | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| **TCRA** | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| **UAE** | United Arab Emirates |
| **UDHR** | Universal Declaration of Human Rights |
| **UN** | United Nations |
| **UNAMID** | United Nations–African Union Hybrid Operation in Darfur |
| **UNAMISS** | United Nations Mission in South Sudan |
| **UNDP** | United Nation Development Programme |
| **UNESCO** | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization. |

# UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU

| NA | NENO | UFAFANUZI |
|---|---|---|
| 1 | Diaspora | Mtu binafsi au raia wa nchi fulani ambaye huhama na kwenda kuishi katika nchi nyingine huku akiendelea kudumisha uhusiano na upendo kwa nchi yake ya asili. Mtu wa aina hii daima atakuwa na mtazamo/nia chanya ya kufuatilia shughuli za maendeleo ya nchi yake ya asili.<br><br>Kwa muktadha wa sera hii, Diaspora ni watu wanaotoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wanaishi katika nchi za nje lakini wanadumisha uzalendo kwa nchi yao. |
| 2 | Diaspora Raia wa Tanzania | Mtu mwenye uraia wa Tanzania anayeishi na kufanya kazi nje ya nchi. |
| 3 | Diaspora Asiye Raia wa Tanzania | Raia wa Nchi Nyingine Mwenye Asili ya Tanzania |
| 4 | Diplomasia ya Uchumi | Shughuli ya kidiplomasia ambayo inakuza uhusiano wa serikali unaozingatia masilahi ya kiuchumi. |

| NA | NENO | UFAFANUZI |
|---|---|---|
| 5 | Uchumi wa Buluu | Shughuli za kiuchumi zinazohusiana na matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na maji safi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi huku zikizingatia uhifadhi wa mazingira. |
| 6 | Uhusiano wa Kimataifa | Mtangamano na uhusiano kati ya nchi moja na nyingine, pamoja na ushirikiano ndani ya mifumo ya kikanda na mashirika ya kimataifa. |
| 7 | Ushirikiano wa Nchi za Kusini | Inamaanisha ushirikiano wa kitaalamu kati ya nchi zinazoendelea katika Ulimwengu wa Kusini hasa Afrika, Asia, Amerika Kusini na Karibiani. |
| 8 | Nchi zisizofungamana na Upande Wowote | Ni jukwaa la nchi ambazo hazijafungamana rasmi na au dhidi ya nchi zenye nguvu kubwa au kundi la nchi hizo. |
| 9 | Ushirikiano wa Kikanda | Ni mchakato wa ushirikiano na uratibu kati ya nchi jirani ili kufikia malengo ya pamoja. |
| 10 | Uhusiano wa uwili | Uhusiano wa kisiasa, kiuchumi, kijamii au kiutamaduni kati ya nchi mbili huru. |
| 11 | Ushirikiano wa kimataifa | Inamaanisha ushirikiano kati ya mataifa mengi au kundi la mataifa yanayofanya kazi pamoja kushughulikia masuala yenye maslahi ya pamoja. |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Usuli

Kufuatia kuzaliwa kwake baada muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kuwa Jamhuri Moja iliyoungana na yenye Mamlaka kamili mnamo mwaka 1964, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ilifafanua maudhui, namna ya kuyaainisha na utaratibu wa kuendesha uhusiano wa kimataifa ili kuongoza ushiriki wake katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

Uendeshaji wa masuala ya kigeni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulijikita katika misingi ya kutofungamana na upande wowote, umoja wa Afrika, uhuru, usawa, kufungamana kwa masilahi nchi huru , na kuheshimu utu na haki za binadamu. Misingi hii imejenga msingi wa uanzishwaji wa uhusiano wa kirafiki na nchi nyingine sambamba na mashirika ya kikanda na ya kimataifa. Vilevile, Sera ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliathiriwa na msingi wa kisiasa wa haki ya Waafrika kujitawala wenyewe. Sera hii iliongoza harakati za ukombozi wa maeneo ya Afrika yaliyokuwa chini ya utawala wa kikoloni, ukombozi wa watu waliodhulumiwa, na kuendeleza umoja wa Afrika.

Kwa muktadha huo,utekelezaji wa masuala yanayohusu uhusiano wa kimataifa uliongozwa na Waraka wa Rais Namba 2 wa Mwaka 1964, Azimio la Arusha la mwaka 1967 na Sera Mpya wa Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, ikiwa ni pamoja na misingi ya kimataifa iliyomo kwenye Mikataba ya Vienna ya mwaka 1961 na 1963 mtawalia. Hivyo, Sera Mpya ya Mambo ya Nje iliundwa ili kukabiliana na mabadiliko ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo yalianza kujitokeza katikati mwa miaka ya 1980, ikiwemo uhitaji wa kufungamana na mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, pamoja na kuongezeka kwa kasi ya utandawazi.

Masuala mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na mabadiliko ya mwenendo wa uchumi wa dunia kuelekea nguvu ya soko; kuongezeka kwa ushirikiano wa Kikanda barani Afrika; mabadiliko ya uhusiano wa kimataifa kutoka utegemezi wa misaada kwenda katika ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi; dhamira ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; maendeleo ya sayansi na teknolojia; kuibuka upya kwa migogoro ya ndani ya nchi na kuongezeka kwa uhalifu wa kuvuka mipaka. Hivyo, Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 iliifanya diplomasia ya uchumi kuwa kiini cha uhusiano wa kimataifa, huku ikidumisha misingi ya jadi ya Sera ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

Katika kipindi cha miongo miwili kuanzia mwaka 2001, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Sera hii kwa kuimarisha uhusiano wa uwili, kuongeza kasi ya ushirikiano wa kikanda na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa. Mafanikio hayo yalichangiwa na kuimarika kwa uhusiano wa kibiashara na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi katika sekta mbalimbali. Kwa ujumla wake, hayo yalichangia kuboresha ustawi wa jamii, maendeleo ya watu, uzalishaji mali na kuondoa umaskini. Vilevile, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshiriki kikamilifu katika taasisi za kikanda na kimataifa. Hii inadhihirishwa na kuongezeka ushiriki wa Tanzania katika kulinda amani na usalama Afrika na nchi mbalimbali duniani.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio makubwa, utekelezaji wa Sera ya Mpya ya Mambo ya Nje uliathiriwa na uhalifu wa unaovuka mipaka ya nchi; kukosekana kwa utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika baadhi ya nchi na mapungufu katika kuchangamkia fursa za mikataba na makubaliano ya kimataifa Aidha, Sera haikuwa imejumuisha mwongozo kuhusu baadhi ya masuala kama vile diaspora, hususan ushiriki wa Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania katika maendeleo ya Taifa;

kutotumia Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia, na matumizi ya rasilimali za baharini kupitia maendeleo ya uchumi wa buluu.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika nyanja za kisiasa, kama vile udugu, ujirani mwema na kuishi pamoja kwa amani ndani ya eneo kikanda, sambamba na kuimarika kwa amani na usalama duniani; mafanikio haya yanatishiwa na mabadiliko hasi ya mienendo ya siasa za kijiografia duniani. Kwa muktadha huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapaswa kujipanga katika uhusiano wa kimataifa, ikiweka mbele diplomasia ya uchumi; amani, usalama, na utulivu wa kisiasa, huku ikichukua hatua stahiki kurekebisha mapungufu yaliyoainishwa na kukabiliana na changamoto mpya.

Kwa mintaarafu hiyo, Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 imefanyiwa mapitio ili kutoa fursa ya mwongozo mpya wa nchi katika uhusiano wa kimataifa na ushirikiano wa kidiplomasia kukabiliana na changamoto zilizokuwepo na zile zitakazoibuka, huku ikitumia ipasavyo fursa zinazotokana na ushirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na kimataifa.

## 1.2. Hali Ilivyo

Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 ilitekelezwa kupitia Mikakati wa Utekelezaji wa Sera wa Mwaka 2004. Mkakati huo ulijielekeza katika maeneo ya kukuza ujirani mwema; kuimarisha amani na usalama wa kikanda; kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda; kuendeleza Umoja wa Afrika; kuendeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote; kukuza ushirikiano wa nchi zinazoendelea; kuimarisha ushiriki katika Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa; kushughulikia masuala ya fedha na deni la Taifa nje; kushirikiana na kampuni za kimataifa; kuunga

mkono Asasi za Kiraia zenye ufanisi; kuweka mazingira wezeshi ya ndani; kuweka kipaumbele katika diplomasia ya uchumi na kufasiri upya diplomasia ya uwili.

### 1.2.1. Mafanikio ya Utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001

Ili kufikia malengo ya kimkakati ya Sera, Serikali, kwa kushirikiana na wadau ilitumia nyenzo mbalimbali za kimataifa kutekeleza hatua na afua zifuatazo:

### 1.2.2. Kuimarika kwa Uhusiano wa Uwili

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliendeleza uhusiano wa uwili kupitia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya ushirikiano, kama vile Mkataba baina ya Shirikisho la Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA) na Jumuiya ya Biashara ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE); uteuzi wa Makonseli wa heshima; kuanzishwa kwa Tume za Pamoja za Ushirikiano (JPC/JCC) na nchi nyingine zikiwemo Afrika Kusini, Angola, Burundi, Brazil, India, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Ufaransa, Uganda, Vietnam na Zambia; na ushiriki katika mashauriano ya kisiasa, usuluhishi wa migogoro na upatanishi.

Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika kampeni mbalimbali za kuvutia utalii na maonesho ya biashara, ikiwemo maandalizi ya filamu ya *Tanzania: The Royal Tour* ya mwaka 2022, Maonesho ya Dubai (2022), Mkutano Maalum wa Kahawa na Maonesho nchini Japani (2022), Wiki ya Tanzania nchini Kenya (2018), Maonesho ya Uhispania (2010), na Maonesho ya Japani (2005). Pia, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikamilisha na kuanza kutekeleza Mikataba ya Kuondoa Utozaji wa Kodi Mara Mbili na nchi za Afrika Kusini

mwaka 2005 na India mwaka 2011, pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa kigeni nchini. Kutokana na juhudi hizo, kati ya mwaka 2015 na 2020, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivutia miradi uwekezaji ikiwemo zaidi ya 464 kutoka Jamhuri ya Watu wa China (PRC), ambayo iliibua fursa za ajira zaidi ya 50,241 katika sekta mbalimbali.

### 1.2.3. Kuimarika kwa Mtangamano wa Kikanda

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mafanikio katika mtangamano wa kikanda kama ifuatavyo:

**Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Kuanza kwa utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2005 na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki mwaka 2010 kumewezesha usafirishaji huru wa bidhaa, huduma, nguvu kazi na mitaji sambamba na haki ya kuanzisha makazi; uingiaji na utokaji huru wa watu; kuanzisha biashara; kurahisisha biashara na uwekezaji wa kuvuka mipaka. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini Itifaki ya Umoja wa Fedha ya mwaka 2013 ambayo inarahisisha utekelezaji wa mpango kazi wa kuanzisha Umoja wa Kifedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuanzishwa kwa sarafu moja ifikapo mwaka 2031; kuitangaza Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kama eneo moja la biashara na uwekezaji, huku ikihakikisha kila Nchi Mwanachama inaendelea na umiliki wa rasilimali zake na kutoa vivutio vya uwekezaji.

Kwa upande wa masuala ya kisiasa, Tanzania ilishiriki katika juhudi za upatanishi na usuluhishi wa migogoro katika eneo la kikanda na utatuzi wa vikwazo vya kisiasa kupitia Jumuiya. Aidha, Tanzania imehusika katika juhudi za kisiasa na za kulinda amani katika eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Vilevile, Tanzania iliongoza

juhudi za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika vyombo vya maamuzi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**

Chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Tanzania hushiriki katika utekelezaji wa programu za mtangamano katika nyanja mbalimbali ikiwemo amani,usalama na utawala bora; maendeleo ya viwanda na mtangamano wa soko; maendeleo ya miundombinu; chakula, kilimo na maliasili; usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake; na maendeleo ya vijana. Mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha ushiriki katika programu za mafunzo za kikanda za ulinzi wa amani kupitia SADC-RCTC na misheni ya ulinzi wa amani wa jumuiya ya kikanda, hasa misheni ya SADC wa ulinzi wa amani nchini Msumbiji (SAMIM), pamoja na kushiriki katika juhudi za kisiasa na diplomasia katika nchi zenye migogoro. Aidha, mwaka 2019, Tanzania iliongoza juhudi za kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya kazi katika Jumuiya.

**Jumuiya ya Nchi Zilizo Mwambao wa Bahari ya Hindi**

Kwa upande wa Jumuiya ya Nchi Zilizo Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA), Tanzania inashiriki katika kutekeleza programu mbalimbali za mtangamano kama vile: uondoaji wa majeshi katika Bahari ya Hindi, ukuzaji uchumi wa buluu, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari; na kuendeleza juhudi za uhifadhi wa mazingira.

**Ushirikiano wa Utatu wa COMESA - EAC – SADC**

Katika kushughulikia suala la mwingiliano wa uanachama kwenye jumuiya zaidi ya moja, Tanzania inaunga mkono juhudi za kuunganisha programu za mtangamano wa jumuiya za kikanda za ushirikiano wa kiuchumi kwa ajili ya watu wa

ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika, ambao unajumuisha Jumuiya za COMESA-EAC-SADC, Utatu wenye Nchi Wanachama 26.

Katika utaratibu huo, Tanzania inanufaika na programu za mtangamano wa soko; maendeleo ya miundombinu na maendeleo ya viwanda. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza kufanya kazi kwa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani (OSBPs) na kuwezesha uingiaji na utokaji huru wa watu; usafirishaji wa bidhaa na kuwezesha biashara ya huduma. Programu hizi zinachangia katika kufanikisha malengo mapana ya Umoja wa Afrika ambayo ni kuongeza kasi ya mtangamano wa kiuchumi ndani ya bara la Afrika na kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi. Aidha, jitihada hizi zinalenga kupunguza umaskini na kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi.

Hivyo, utekelezaji wa Makubaliano ya Utatu huu pia yanalenga kufikia malengo ya Makubaliano ya Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), ikijumuisha usimamizi wa itifaki mbalimbali katika maeneo ya biashara za bidhaa na huduma, usuluhishi wa migogoro ya forodha na uwezeshaji wa biashara. Maeneo mengine ni pamoja na haki miliki, uwekezaji, sera ya ushindani, biashara ya kidijiti na ushiriki wa wanawake na vijana katika biashara.

### 1.2.4. Kuimarikwa kwa Ushirikiano wa Kimataifa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mafanikio mbalimbali kupitia ushirikiano wa kimataifa, yakijumuisha ushiriki katika misheni za kulinda amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa ikiwemo Lebanon, Abyei, Sudan, Darfur, Sudani Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Mafanikio mengine ni kutangazwa kwa tarehe 7 Julai kila mwaka kuwa siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani; kuendeleza maslahi ya Taifa katika majadiliano ya kimataifa kupitia Kundi la nchi 77 na China. Kadhalika, Tanzania imeshiriki katika kuchagiza kuanzishwa kwa muundo wa Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, ambapo mashirika 23 ya Umoja wa Mataifa yanashiriki katika utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo vya Taifa chini ya Mpango Mmoja wa Umoja wa Mataifa. Sambamba na hayo, Tanzania ilipata nafasi mbalimbali za ujumbe katika mashirika na vyombo vya maamuzi kimataifa, ikijumuisha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2005 - 2006), Bodi Tendaji ya UNDP/UNFPA/UNOPS (2016), Kamati ya Programu na Uratibu (2013 – 2015, 2016 - 2018), Baraza la Uchumi na Masuala ya Kijamii Umoja wa Mataifa (2004 – 2006), na kuwa Mratibu katika Kamati ya Utawala na Bajeti ya Mataifa (2012 - 2013). Vilevile, Tanzania, ilikuwa mwenyeji wa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (ICTR) mjini Arusha kuanzia mwaka 1995 hadi ilipofungwa mwezi Desemba mwaka 2015. Kadhalika, Tanzania inaendelea kuwa mwenyeji wa taasisi muhimu za kimataifa na kikanda zikiwemo, *International Residual Mechanism for Criminal Tribunals*, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Umoja wa Posta Afrika, Bodi ya Kuzuia Rushwa ya Umoja wa Afrika na Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa.

### 1.2.5. Kukuza Diplomasia ya Uchumi

Kupitia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanikiwa kudumisha masoko mbalimbali ya jadi ya mauzo ya bidhaa na huduma ikiwemo Umoja wa Ulaya na Marekani, kupitia mpango wa Bidhaa Zote Isipokuwa Silaha (EBA) na Mpango wa Ukuaji wa Afrika na Fursa (AGOA), mtawalia. Aidha, Tanzania imepata masoko mapya ya bidhaa zake ndani ya Afrika, Asia na Mashariki ya Kati. Hatua hizo zimeongeza thamani ya mauzo ya nje kutoka

Dola za Marekani milioni 1,766.7 mwaka 2001 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 11,601.4 mwaka 2022. Kadhalika uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 549.3 mwaka 2001 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,111.5 mwaka 2022. Halikadhalika, ajira zilizotokana na uwekezaji huo ziliongezeka kutoka 98,889 mwaka 2013 hadi kufikia 105,364 kwa mwaka 2017. Vilevile, Tanzania imenufaika na ufadhili wa masomo, uhaulishaji wa teknolojia na fursa za kubadilishana ujuzi na uzoefu wa kitaaluma kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kamatifa.

## 1.3. Changamoto Katika Utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje (2001)

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje (2001) ulikumbwa na changamoto mbalimbali, zikijumuisha zifuatazo:-

### 1.3.1. Kuendelea kuwepo kwa Uhalifu Unaovuka Mipaka

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera hii, mzunguko wa biashara, uwekezaji, ajira na mitaji ulikabiliwa na vikwazo kutokana na uhalifu wa unaovuka mipaka kama vile, usafirishaji haramu wa binadamu, bidhaa za magendo, wanyama, silaha na dawa za kulevya, utakatishaji wa fedha, pamoja na vitisho vya kimtandao vya kimataifa. Changamoto hizi zilidhoofisha fursa za mtangamano imara na wenye tija kimataifa.

Uhalifu unaovuka mipaka unapunguza kasi ya Tanzania kushiriki kikamilifu katika shughuli za biashara na nchi jirani, na hivyo kupelekea matumizi hafifu ya Itifaki za Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uhalifu huu unaleta vitisho vikubwa kwa mikoa ya mipakani

na umeendelea kuleta usumbufu katika biashara. Aidha, hali hii pia inasababishwa na kukosekana kwa utulivu wa kisiasa katika baadhi ya nchi , ambazo huzaa masoko haramu ya bidhaa za magendo, wanyama, silaha na dawa za kulevya.

Kufuatia hali hiyo, Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kupunguza kiwango cha uhalifu zikiwemo, kusaini mikataba na nchi rafiki kuhusu urejeshaji wa watuhumiwa wa ugaidi katika nchi husika, ili kufunguliwa mashtaka au kuanza kutumikia kifungo. Aidha, Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kupeana taarifa muhimu na kufanya operesheni za pamoja dhidi ya ugaidi. Hatua nyingine ni, kuanzishwa kwa Kituo cha Kitaifa cha Kupambana na Ugaidi (NCTC) mwaka 2021; kutunga na kutekeleza Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2008, Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002 na Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu ya mwaka 2022.

Kadhalika, Tanzania imeanzisha taasisi zinazolenga kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu unaovuka mipaka. Taasisi hizo ni pamoja na Mahakama, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) na Sekretarieti ya Kitaifa ya Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu. Nyingine ni, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU), Tume ya Haki za Binadamu (HRC) na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS).

Licha ya jitihada hizo, uhalifu wa kuvuka mipaka unaendelea kufanyika kikanda na kimataifa. Hivyo, diplomasia ya kuzuia migogoro inapaswa kuimarishwa ili kupunguza mizozo inayosababisha kukosekana kwa utulivu wa kisiasa. Wakati huo huo, utekelezaji wa mikataba na itifaki za amani na usalama, pamoja na ushirikiano na mashirika ya kimataifa, ukiimarishwa zaidi ili kupambana na uhalifu wa kuvuka mipaka.

### 1.3.2. Kukosekana kwa Utulivu wa Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa

Mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kikanda na kimataifa yanapelekea ugumu na kutabiri ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uga wa kimataifa. Kukosekana kwa utulivu kwa baadhi ya nchi washirika na wadau wengine wa kimataifa husababisha changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na kuathiri uwezo wa nchi kunufaika ipasavyo na fursa zilizopo. Hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na changamoto ya kutofaidika kikamilifu na mazingira ya nje yaliyoathiriwa na kudhoofika kwa demokrasia na utawala wa sheria, viwango vya juu vya ukosefu wa ajira, umaskini, ubaguzi wa rangi na machafuko yaliyokithiri katika baadhi ya nchi.

Kwa mintaarafu hiyo, ili kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika ngazi za kikanda na kimataifa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa ikiwemo, Mkataba wa Vienna wa mwaka 1961 na 1963 kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia. Aidha, katika kuimarisha uhusiano wa kisiasa, kijamii na kiuchumi, hadi mwaka 2024 Tanzania ilikuwa imeanzisha Balozi 45 na Konseli Kuu tano (5) kwa ajili ya kuimarisha uhusiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Mafanikio mengine ni kuchangia katika usuluhishi wa migogoro katika eneo la Afrika.

Kadhalika, ili kuwezesha ushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini Mikataba na Umoja wa Mataifa inayohusiana na kuchangia Vikosi vya Jeshi na Polisi pamoja na Vifaa Vinavyomilikiwa na Vikosi vya Nchi Wanachama (COE), kwa mujibu wa masharti Mahsusi yaliyoainishwa kupitia maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ikiwemo Azimio Namba 71/296. Kupitia Makubaliano hayo, Tanzania ilishiriki katika Misheni za kulinda amani za

Umoja wa Mataifa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (MONUSCO), Lebanon (UNIFIL), Sudan Kusini (UNAMISS), Abyei (UNISFA), Jamhuri ya Afrika ya Kati (MINUSCAR) na Misheni ya Kulinda Amani ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika Jimbo la Darfur (UNAMID). Vilevile, Tanzania iliongoza uanzishwaji wa Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha SADC (SADC-RCTC) ili kutambua viashiria, kuzuia na kupambana na ugaidi, ambao ni tishio mojawapo la utulivu kwenye eneo la kikanda. Hata hivyo, licha ya juhudi hizi, hali ya kutokuwepo kwa utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika baadhi ya nchi bado inaendelea. Hivyo, hatua zaidi zinahitajika ili kujenga na kuimarisha utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa.

### 1.3.3. Changamoto Katika Kuridhia Mikataba na Itifaki Zilizosainiwa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mikataba kadhaa ya sheria za kimataifa ili kuongeza kasi ya mtangamano na ushiriki katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

Hata hivyo, yapo mapungufu yanayohusiana na kuridhia mikataba ya kimataifa, ikiwemo ukosefu wa mpango unaoainisha muda maalumu wa kukamilisha mchakato wa kuridhia hatua inayotokana na hitaji la ushirikishwaji wa wadau kikamilifu na hivyo kuchukua muda mrefu. Uhusiano wa kimataifa ulio madhubuti na wenye tija hutegemea umuhimu na utekelezaji wa mikataba na itifaki husika. Hivyo, kuridhia mikataba hiyo inatoa nafasi kwa nchi kunufaika ipasavyo na fursa zilizomo katika ushirikiano husika.

Hata hivyo, ipo baadhi ya mikataba na Itifaki za kimataifa iliyosainiwa ambayo bado haijaridhiwa. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Kuzuia Utozaji Kodi Mara Mbili na Kudhibiti Ukwepaji Kodi ya Mapato wa

mwaka 2010; Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uratibu wa Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2010 na Itifaki ya SADC ya Biashara ya Huduma ya 2012. Kwa ujumla, kutokukamilika kwa hatua za kuridhia mikataba hii ya kimataifa kunapunguza kasi ya kupata manufaa husika ikiwemo uwekezaji na mtiririko wa mtaji kwa nchi wanachama na kupunguza tija katika biashara ya huduma.

Kwa msingi huo, ni muhimu kuboresha taratibu za kitaalamu za kushughulikia mikataba ya kimataifa kwa kuzingatia muda unaohusika. Aidha, kuimarisha mifumo madhubuti ya uratibu na uchambuzi wa mikataba hii kutaongeza ufanisi katika kubaini manufaa na hivyo kuiwezesha nchi kunufaika kikamilifu kiuchumi.

### 1.3.4. Mwingiliano wa Uanachama Katika Jumuiya za Kikanda na Taasisi za Kimataifa.

Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa, kama vile EAC, SADC, IORA na ICGLR. Kuwa mwanachama katika taasisi za kikanda na kimataifa kunatoa fursa ya ushirikiano katika mtangamano. Hata hivyo, mwingiliano wa uanachama wenye malengo yanayofanana husababisha wajibu unaokinzana, ambao huambatana na gharama zinazohusiana na mwingiliano huo.

Licha ya uwepo wa faida kadhaa zilizobainishwa kuhusu uanachama katika jumuiya ya kikanda na kimataifa, mwingiliano wa uanachama huleta changamoto katika utekelezaji wenye tija wa mikataba mbalimbali. Mathalani, Tanzania kuwa Nchi Mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, inanufaika na utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya EAC huku ikikabiliwa na changamoto katika kutekeleza kwa ukamilifu Itifaki ya Umoja wa Forodha ya SADC kutokana na uanachama

wake katika SADC, ambao uko katika hatua ya Eneo Huru la Biashara (SADC-FTA).

Hivyo, ni muhimu kujenga ushirikiano wa pamoja kati ya jumuiya husika za kiuchumi za kikanda ili kufikia manufaa yaliyokusudiwa kutoka katika miungano mbalimbali. Kwa muktadha huo, utekelezaji wa makubaliano ya Mpango Utatu wa COMESA-EAC-SADC na Eneo Huria la Biashara la Bara la Afrika yanatarajiwa kutatua changamoto ya mwingiliano wa uanachama. Hatua hizo zitaboresha nafasi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uhusiano huo.

### 1.3.5. Matumizi Hafifu ya Kiswahili katika Diplomasia

Kiswahili ni lugha ya Taifa na moja ya lugha zinazozungumzwa na watu wengi duniani. Umoja wa Mataifa unakadiria kuwa, kuna wazungumzaji wa Kiswahili zaidi ya milioni 500 duniani kote. Aidha, kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuna zaidi ya vyombo vya habari 1,422 duniani kote vinavyotoa maudhui kwa lugha ya Kiswahili na kwamba, lugha hiyo inafundishwa katika taasisi za elimu ya juu zaidi ya 150 duniani.

Kiswahili kimetambulika kama nyenzo ya kuongoza diplomasia na biashara katika ngazi zote pamoja na kutatua migogoro na kufanya upatanishi. Kiswahili kimetumika kama nyenzo ya ukombozi na mapambano ya uhuru, utambulisho wa Taifa, utu na lugha ya kuleta mshikamano kwa waafrika wote na watu wenye asili ya Afrika duniani kutoka maeneo mbalimbali kama vile Marekani, Karibe na Ulaya. Ingawa Tanzania imekuwa ikitumia Kiingereza kama lugha kuu ya diplomasia, jitihada za hivi karibuni zinasisitiza matumizi ya Kiswahili. Mfano wa matumizi ya Kiswahili katika matukio ya kimataifa umeonekana katika kuhutubia mikutano ya ngazi ya juu ya SADC, EAC na Umoja wa Afrika kwa lugha ya Kiswahili.

Hatua hii muhimu ilifikiwa kwa kuanza kutumika rasmi kwa Kiswahili kama Lugha Rasmi ya Nne ya SADC wakati wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Agosti 2019, Lugha Rasmi ya EAC wakati wa Mkutano wa 21 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi za EAC, mwezi Februari mwaka 2021 na Lugha Rasmi ya Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Februari 2022.

Aidha, katika kikao cha 41 cha Mkutano Mkuu wa mwaka 2021, wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) uliridhia Azimio Na. 41C/61 la kutambua mchango wa lugha ya Kiswahili katika kukuza utamaduni, kujenga uelewa na majadiliano ya kiutamaduni. Azimio hilo lilitangaza kuwa tarehe 7 Julai kila mwaka itakuwa Siku ya Lugha ya Kiswahili Ulimwenguni. Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Afrika kupokea utambulisho huo kutoka Umoja wa Mataifa.

Licha ya mafanikio haya, bado kuna matumizi hafifu ya Kiswahili, hususan katika majadiliano ya mikataba ya ushirikiano ya kimataifa, pamoja na mazungumzo ya kitaalamu katika maeneo mbalimbali yenye maslahi. Aidha, thamani ya kiuchumi ya Kiswahili haijatambuliwa ipasavyo ikilinganishwa na unavyotambuliwa umuhimu wake wa kitamaduni. Hivyo, jitihada zaidi na mikakati sahihi inahitajika ili kukuza matumizi ya Kiswahili katika majadiliano ya mikataba ya kimataifa na kuimarisha nafasi yake kama lugha ya diplomasia katika uhusiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

### 1.3.6. Changamoto katika Uratibu wa Utekelezaji

Ufanisi katika utekelezaji wa sera unategemea uratibu thabiti wa wadau ili kuepuka migongano na mwingiliano wa afua. Muundo wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu unawezesha uratibu wa ushirikiano wa uwili, kikanda na

kimataifa ili kuwezesha utekelezaji wa sera. Kiutendaji, uratibu unafanyika kwa maeneo mahsusi ya kijiografia, kikanda na kimataifa.

Japokuwa, kuna uhusiano imara wa kimuundo kwa Idara, Wizara na Taasisi za Serikali bado kumekuwepo na changamoto katika uratibu wa utekelezaji wa Sera. Hii inasababisha kutokutekelezwa ipasavyo kwa baadhi ya afua za sera. Kwa muktadha huo, kuna umuhimu wa kuimarisha uratibu wa wadau katika ngazi zote ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sera.

### 1.3.7. Mapungufu Katika Utafutaji wa Rasilimali

Utafutaji jumuishi na wenye ufanisi wa rasilimali unahitaji utambuzi na matumizi bora ya rasilimali watu, teknolojia na mtaji. Kimsingi, tija katika utafutaji wa rasilimali inatokana na makubaliano yanayowaweka wadau katika nafasi ya kunufaika na uhusiano maalumu wa kimataifa. Katika muktadha huu, rasilimali huchukuliwa kama hitaji la msingi la kuwezesha ushiriki wenye mantiki katika masuala ya kimataifa.

Katika utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, utafutaji rasilimali umechangia kwa kiasi kikubwa katika kufadhili bajeti ya Serikali hususn utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo, ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imenufaika na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje, msamaha wa madeni na msaada wa kitaalamu. Aidha, Tanzania ilinufaika na programu za mafunzo na kubadilishana uzoefu na ujuzi.

Katika kuchangia jitihada za kutafuta rasilimali, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kama vile, kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Deni wa Muda wa Kati; kufanya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Taifa, kuanzisha Mfumo Jumuishi wa

Usimamizi wa Mapato ya Ndani; utekelezaji wa Sheria ya Bajeti; Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada na maandalizi ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (2017/18 – 2024/25) kama nyenzo za kuongoza ushirikiano wa Tanzania na wadau wa maendeleo katika ugharamiaji wa maendeleo; utoaji wa taarifa kwa umma kuhusu fursa za kuboresha rasilimali watu kupitia mafunzo na uhawilishaji wa teknolojia hususan katika miradi ya maendeleo.

Hili liliwezeshwa na programu za mafunzo na vipengele vya uhamishaji wa teknolojia wakati wa utekelezaji wa miradi ya sayansi na teknolojia, kwa lengo la kuendeleza rasilimali watu, hususan katika ujuzi wa kitaalamu na wa ufundi.

Aidha, Serikali kupitia Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa maendeleo ya Taifa ilijumuisha ajenda za kimataifa kama vile Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu; Ajenda 2063: "Afrika Tuitakayo" ya Umoja wa Afrika ili kuoanisha mfumo wa maendeleo wa nchi na malengo ya kimataifa. Hili linaakisiwa katika Mfumo Jumuishi wa Ufadhili wa Maendeleo ya Taifa (INFF), ambao unaoanisha ufadhili wa mipango ya maendeleo ya Taifa na malengo endelevu kwa kuzingatia mwongozo wa Ajenda ya Addis Ababa ya mwaka 2015 kuhusu ufadhili wa malengo endelevu.

Hata hivyo, licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kurekebisha mawanda ya mfumo wa kimataifa wa kifedha, ukusanyaji wa rasilimali bado una changamoto mbalimbali ikiwemo muundo usiotabirika wa ufadhili wa kimataifa; mabadiliko ya mara kwa mara ya vigezo na masharti ya kupata rasilimali fedha na kubadilika kwa vipaumbele viliyowekwa na baadhi ya wabia wa maendeleo.

Hali hii husababisha upungufu, ucheleweshwaji wa upatikanaji wa rasilimali kutoka nje. Hivyo, kwa kuwa , Sera ya Mambo ya

Nje ya Mwaka 2001 inasisitiza zaidi kuhusu utafutaji wa rasilimali fedha pasipo kuainisha aina nyingine za rasilimali, mabadiliko yanayoibuka hivi sasa yanahitaji kujumuishwa kwa rasilimali zisizo za kifedha, kama vile rasilimali watu na teknolojia, kama michango muhimu katika maendeleo.

Kwa muktadha huo, ubunifu zaidi unapaswa kutumika katika utafutaji wa rasilimali kimataifa, kwa kuendeleza vyanzo vya jadi na kusisitiza vyanzo vingine vipya, ikiwemo hatifungani za diaspora, uuzaji wa kaboni na hati fungani za uhifadhi wa mazingira na bioanuwai. Aidha, rasilimali watu, uhawilishaji wa teknolojia na ushirikiano wa kimkakati vinapaswa kuunganishwa kama sehemu ya vyanzo hivyo, ili kuchangia ipasavyo katika ajenda ya maendeleo ya Taifa.

## 1.4. Masuala Mapya ya Kisera

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, masuala mapya yalibainika na hivyo kuathiri utekelezaji wake. Masuala ambayo hayakuwa na miongozo ya kisera kuyashughulikia katika uhusiano wa kimataifa ni pamoja na:-

### 1.4.1. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Madhara ya uchafuzi wa mazingira, upotevu wa bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi yamekuwa ni sehemu ya changamoto kubwa iliyoenea nchini na duniani kote. Athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi zimejidhihirisha katika sekta zote nchini. Mathalani, matukio ya hali ya hewa yaliyotokana na mabadiliko ya tabianchi ni kama vile ukame, upepo mkali, vipindi virefu vya kukosa mvua, mvua zisizotabirika, mabadiliko ya misimu ya mvua na mafuriko. Hali hii imesababisha kuongezeka

kwa uhaba wa maji, kupungua kwa usalama wa chakula, kuenea kwa jangwa na mabadiliko ya mfumo wa ikolojia. Aidha, ongezeko la kina cha maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi limesababisha kuzama kwa baadhi ya visiwa na kuingia kwa maji ya bahari katika visima pamoja na uharibifu wa shughuli nyingine kwenye fukwe.

Tanzania imechukua hatua kadhaa katika kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na, kutunga Sera ya Taifa ya Mazingira; kutunga Sheria ya Mazingira na kanuni zake; kuridhia na kuanza kutekeleza mikataba mbalimbali ya mazingira kikanda na kimataifa na kutunga na kutekeleza miongozo, mikakati na programu kama vile Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Afua za Kimkakati za Mazingira (2022-2032), Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026) na Mpango wa Mchango wa Taifa wa Kupunguza Gesi Chafuzi (2021).

Licha ya jitihada hizo, changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi zimeendelea kuwepo. Hii inajenga msingi wa kuongeza jitihada katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, jitihada hizo zinakumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo, upatikanaji mdogo wa fedha na teknolojia kutoka katika mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii inahitaji ushiriki madhubuti wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majukwaa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa majadiliano na kujenga hoja ili kupata rasilimali fedha na teknolojia za ugharamiaji wa athari za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

### 1.4.2. Ushirikishwaji na Ushiriki wa Diaspora

Diaspora wanachukuliwa kama kichocheo muhimu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi zao za asili. Hivyo,

ushiriki wao ni sehemu muhimu ya uhusiano wa kimataifa wa nchi. Kwa mantiki hiyo, umuhimu wa mchango wa Diaspora katika maendeleo ya Taifa hauwezi kupuuzwa. Hata hivyo, kumekuwepo na mapungufu katika mbinu za kuwashirikisha na kufaidi michango inayotokana na shughuli za jumuiya ya diaspora.

Hivyo, ili kuhakikisha ushirikishwaji na ushiriki wa Diaspora katika uhusiano wa kimataifa, Serikali ilianzisha Idara ya Diaspora chini ya Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hatua hii inalenga kuongeza tija katika ushiriki wa diaspora kwenye maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, ushirikishwaji wa diaspora ulikuwa na upungufu wa msingi wa sera nje ya nchi. Aidha, zipo jumuiya za diaspora ambazo zimesajiliwa katika nchi wanazoishi. Jumuiya hizo ni sehemu ya wadau wa serikali katika ushirikishwaji wa diaspora kwenye nchi mwenyeji. Kwa muktadha huo, ni muhimu kwa Tanzania kuweka utaratibu wa kisera utakaowezesha ushiriki wa hali ya juu wa diaspora katika maendeleo ya Taifa. Hili litawezekana kwa kuweka mwelekeo maalumu wa kisera wa kutoa baadhi ya haki na upendeleo maalumu kwa diaspora ambao ni Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania ili kuwezesha ushiriki wao katika maendeleo ya Taifa lao la asili. Vilevile, shughuli za diaspora zihamasishwe kuwa sehemu ya ajenda ya maendeleo ya Taifa, kujenga taswira nzuri ya Tanzania duniani na kusaidia juhudi za kukuza biashara, uwekezaji, utalii na utamaduni.

### 1.4.3. Msisitizo wa Diplomasia ya Uchumi

Diplomasia ya uchumi ni nyenzo inayotumiwa katika uhusiano wa kimataifa ili kuendeleza maslahi ya Taifa ya kiuchumi. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza utumiaji wa diplomasia ya uchumi katika uhusiano wa kimataifa ili kunufaika na faida mbalimbali kama vile teknolojia mpya, masoko ya nje, uwekezaji

wa moja kwa moja kutoka nje, misaada na mikopo yenye masharti nafuu, kuvutia utalii na kutengeneza ajira. Ili kufikia manufaa yaliyokusudiwa, Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 inasisitiza ujumuishaji wa maslahi ya kiuchumi katika uhusiano wa kimataifa. Katika kutekeleza suala hilo, Serikali ilianzisha Idara inayohusika na Diplomasia ya Uchumi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa lengo la kuimarisha uratibu, uchambuzi na kuhakikisha maslahi ya kiuchumi yanazingatiwa katika uhusiano wa kimataifa.

Hata hivyo, licha ya juhudi za kuweka kipaumbele katika diplomasia ya uchumi, bado kuna mapungufu katika utekelezaji kwenye sekta mbalimbali, ambayo yanahitaji juhudi za kisera kuyaboresha. Kwa muktadha huo, Sera imeweka mwongozo utakaowezesha sekta husika kufafanua majukumu na wajibu wao katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Vilevile, Balozi za Tanzania nje ya nchi zinahitaji kuwa na utaratibu maalum wa kubaini maslahi ya fursa za kiuchumi kwa wigo mpana katika maeneo yao ya uwakilishi.

### 1.4.4. Haki za Binadamu na Utawala Bora

Tanzania inazingatia misingi ya haki za binadamu na utawala bora kwa kuhakikisha utu na haki nyingine za binadamu zinaheshimiwa na kuenziwa. Masuala haya yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sehemu ya Pili na ya Tatu kuhusu Haki na Wajibu wa Msingi, hususan Ibara ya 29 (1) inayotamka kuwa "Kila mtu katika Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu, na matokeo ya kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii."

Aidha, Tanzania inazingatia haki za binadamu kwa mujibu wa mikataba na itifaki za kimataifa za haki zakiraia na kisiasa. Kwa

muktadha huo, Tanzania imesaini nyenzo za kikanda na kimataifa ikijumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 1945 na kuridhia Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) la Mwaka 1948; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Vienna kuhusu Sheria ya Mikataba wa Mwaka 1969. Tanzania pia imesaini Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 na Mkataba wa SADC wa Haki Muhimu za Kijamii wa 2003.

Vilevile, Tanzania imeweka utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na utoaji taarifa kuhusu masuala ya haki za binadamu. Taratibu hizo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Haki na Wajibu Muhimu ya mwaka 1994, Sheria ya Utajiri na Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017, na uanzishwaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Idara huru ya Serikali, kukuza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Hali kadhalika Tanzania inatoa fursa kwa wadau wa nje ya Serikali kama vile vyombo vya habari, AZAKI na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu masuala ya haki za binadamu nchini.

Zaidi ya hayo Tanzania hutoa taarifa ya masuala ya haki za binadamu katika ngazi za Taifa, kanda na kimataifa. Mathalan, utoaji wa taarifa kwa Mapitio ya Hali ya Haki za Binadamu inayowasilishwa katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Kuzingatia haki za binadamu hutoa fursa kwa Tanzania kuweza kushiriki kikamilifu, kwa kujiamini katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kuzingatia mila, desturi na tamaduni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 1.4.5 Jinsia na Vijana

Ujumuishwaji wa masuala ya jinsia na ushirikishwaji wa vijana ni mambo ya kimkakati yanayosisitizwa katika Sera. Msingi wa ujumuishwaji huu unatokana na umuhimu wa vijana kuwa sehemu kubwa ya idadi ya watu nchini na kwa kuzingatia mchango wao wa kiuchumi katika Taifa, huku ujumuishaji wa masuala ya kijinsia ukilenga kuhakikisha usawa wa jinsia katika mageuzi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera, Tanzania imeshuhudia ufungamanishaji wa masuala ya jinsia katika sera za ndani za nchi, ambapo nyenzo zote za utekelezaji zilitakiwa kuzingatia suala hilo. Kwa upande wa vijana, Serikali na wadau wanatambua vijana kama chachu ya mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Serikali inaamini kuwa jitihada zilizofanyika kuhusu ajenda za jinsia na vijana ni zenye manufaa, kwa kuwa masuala haya yanaendelea kupewa umuhimu katika ushirikiano wa kimataifa. Hii inadhihirishwa na takwa la kujumuisha mahitaji ya vijana ili kwenda sambamba na mabadiliko ya dunia. Kwa muktadha huo, ni muhimu kuweka mikakati ya kuzingatia usawa wa jinsia na fursa kwa vijana katika ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

# SURA YA PILI

# MSINGI, DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA

## 2.1. Msingi

Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 inatoa mwongozo katika usimamizi wa masuala ya mambo ya nje. Sera hiyo inaangazia kufikia maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kupitia diplomasia ya uchumi inayolenga kuhakikisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine na mashirika ya kimataifa unazingatia maslahi ya kiuchumi. Malengo mengine ni; kujenga uchumi unaojitosheleza na endelevu, kulinda amani na usalama wa taifa pamoja na kuunga mkono juhudi za kikanda na kimataifa za kuwa na dunia bora na yenye amani. Aidha, Sera imejielekeza kwenye kuongeza kasi ya mtangamano wa kikanda katika siasa, jamii na uchumi; na kuweka mazingira wezeshi kwa Tanzania kushiriki ipasavyo katika majadiliano ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa.

Pamoja na  mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Sera, juhudi za pamoja zinahitajika ili kuboresha dhana ya mambo ya nje. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera, zipo changamoto na fursa ambazo zimeibuka na hivyo kujenga hoja ya kufanya mapitio ya Sera hii. Changamoto hizo ni uwepo wa uhalifu wa mipakani, kukosekana kwa utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa; na mrundikano na mwingiliano wa uanachama wa Tanzania katika taasisi za kikanda na kimataifa. Aidha, utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 uliibua fursa mbalimbali zikiwemo ushiriki wa diaspora katika maendeleo ya Taifa, uchumi wa buluu, matumizi ya Kiswahili katika diplomasia, mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kujumuisha masuala ya jinsia na fursa kwa vijana katika uhusiano wa kimataifa.

Hivyo, mapitio ya Sera yalilenga kuweka malengo na mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizobainika na kuainisha hatua za kisera za kushughulikia  maeneo mapya.

## 2.2. Dira, Dhima na Malengo

### 2.2.1. Dira

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyo salama, shindani na yenye ustawi.

### 2.2.2. Dhima

Kuwezesha na kukuza maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia diplomasia yenye ufanisi.

### 2.2.3. Lengo Kuu

Kuendeleza maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ushirikiano na uhusiano wa kimataifa.

### 2.2.4. Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ni:

i. Kuongeza tija katika matumizi ya fursa za kiuchumi zilizopo katika uhusiano wa kimataifa;

ii. Kulinda amani, usalama na utulivu wa kisiasa;

iii. Kuongeza tija ya matumizi ya itifaki na mikataba ya kimataifa;

iv. Kuimarisha ushirikiano wa uwili;

v. Kuongeza tija katika ushirikiano wa kikanda;

vi. Kutumia kikamilifu fursa zinazotokana na mfumo wa Umoja wa Mataifa na majukwaa mengine ya kimataifa;

vii. Kuongeza matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya kidiplomasia;

viii. Kuimarisha utafutaji na utumiaji wa rasilimali za kimataifa kwa maendeleo ya Taifa;

ix. Kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na vyanzo vingine vya maji;

x. Kuimarisha ushiriki wa diaspora katika maendeleo ya Taifa;

xi. Kusimamia haki za binadamu na utawala bora kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kuzingatia mila na desturi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

xii. Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

xiii. Kuhakikisha ujumuishwaji wa masuala ya jinsia na fursa vijana katika ushirikiano wa kimataifa.

## 2.3. Misingi ya Sera ya Mambo ya Nje

Utekelezaji wa malengo ya Sera ya Mambo ya Nje unaongozwa na misingi ifuatayo:

i. Kulinda Mamlaka kamili ya nchi, mipaka kamili na uhuru wa kisiasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Kulinda uhuru, haki za binadamu, usawa na demokrasia;

iii. Kukuza ujirani mwema;

iv. Kukuza Umoja wa Afrika;

v. Kuongeza ushirikiano wa kiuchumi na washirika wa maendeleo;

vi. Kuwezesha utekelezaji wa sera ya kutofungamana na upande wowote na Ushirikiano wa nchi zinazoendelea;

vii. Kuunga Mkono Umoja wa Mataifa katika kuimarisha maendeleo ya kiuchumi, amani na usalama na

viii. Kulinda maadili, mila, desturi na utamaduni wa watu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# SURA YA TATU

# MASUALA, MALENGO NA MATAMKO YA SERA

# 3.0. Sera

Sura hii inatoa muhtasari wa malengo na Matamko ya Sera yatakayoiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ushirikiano na uhusiano wa kimataifa. Matamko mahsusi ya kisera yanatoa mwongozo kwa wadau wote katika kutumia fursa za kisiasa, kijamii, kiutamaduni na maendeleo ya uchumi na masuala ya mambo ya nje.

## 3.1. Diplomasia ya Uchumi

Uhusiano wa kimataifa unalenga kuwa na faida za kiuchumi kwa pande zote zinazoshiriki. Hii ndiyo sababu uhusiano wa kimataifa huweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi, kuangazia ukuzaji wa biashara, uwekezaji, uhawilishaji wa teknolojia, uendelezaji vipaji, na rasilimali watu, mikutano, utamaduni na utalii, ikijumuisha utalii wa matibabu. Kwa kuzingatia fursa zilizopo, Tanzania inaendeleza diplomasia ya uchumi katika uhusiano wa uwili, kikanda na kimataifa.

Diplomasia ya uchumi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalenga kuimarisha nafasi ya nchi kiuchumi kwa kutumia fursa zinazotokana na ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa husussani Maeneo Huru ya Biashara Barani Afrika. Aidha, Tanzania inaendeleza uhusiano wake na washirika wa jadi kiuchumi, huku ikitafuta masoko mapya, hasa katika nchi za kimkakati zinazoibuka kiuchumi. Kwa sasa, diplomasia ya Tanzania inalenga kujumuisha masuala ya kiuchumi katika nyanja zote za ushirikiano ili kufikia malengo ya Sera.

### 3.1.1. Lengo la sera

Kuongeza matumizi ya fursa za kiuchumi zilizopo katika uhusiano wa kimataifa.

### 3.1.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kutekeleza maslahi ya uchumi yenye matokeo katika uhusiano wa kimataifa;

ii. Kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

iii. Kuendeleza masoko ya jadi na kutafuta masoko mapya; na

iv. Kuhakikisha ushiriki wa Zanzibar katika masuala ya uhusiano wa kimataifa.

## 3.2. Amani, Usalama na Utulivu wa Kisiasa

Amani, usalama na utulivu wa kisiasa ni vigezo muhimu vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mambo yanayosababisha kukosekana kwa amani, usalama na utulivu wa kisiasa ni pamoja na kuporomoka kwa demokrasia na utawala wa sheria, ukosefu wa ajira, umaskini, kuongezeka kwa umiliki haramu wa silaha, makosa ya uhalifu wa kimataifa, ubaguzi wa rangi na vurugu zilizokithiri. Mienendo inayokiuka amani, usalama na utulivu wa kisiasa hudhoofisha uwezo wa nchi katika majadiliano ya kimataifa na kuathiri uwezo wake wa kunufaika na fursa zinazotokana na ushirikiano wa kimataifa.

Kwa muktadha huo, Tanzania itafanya kazi kwa karibu na wadau wote ili kukuza maelewano, utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa pamoja na kuhakikisha amani na usalama kupitia diplomasia ya kuzuia migogoro. Hii ni kwa sababu, uwepo wa amani na utulivu hutoa fursa na mazingira wezeshi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunufaika na ushirikiano wa kimataifa.

### 3.2.1. Lengo la Sera

Kukuza amani, usalama na utulivu wa kisiasa.

### 3.2.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuimarisha ushirikiano na wadau muhimu katika jitihada za kulinda amani na usalama duniani; na

ii. Kuunga mkono juhudi za kurejesha na kudumisha utulivu wa kisiasa duniani.

## 3.3. Mikataba, Makubaliano, Maazimio na Itifaki

Mikataba, makubaliano, maazimio na itifaki ni nyenzo za kimataifa zenye nguvu ya kisheria, ambazo hutoa fursa kwa nchi kunufaika na ushirikiano wa kimataifa na mtangamano wa kiuchumi. Hata hivyo, matumizi bora ya nyenzo hizi hutegemea msimamo wa nchi katika masuala ya uhusiano wa kimataifa na uwezo wake wa kuziweka katika mfumo wa kisheria na kiutendaji ndani ya nchi.

Kumekuwa na changamoto katika kuridhia mikataba ya kimataifa ikiwemo ukosefu wa mpango unaoainisha muda maalumu wa kukamilisha mchakato husika. Hatua hii inachangiwa na hitaji la ushirikishwaji wa wadau kikamilifu na hivyo kuchukua muda mrefu. Kwa msingi huo, ni muhimu kubainisha maeneo ya vipaumbele ipasavyo, kujenga uwezo wa usimamizi na majadiliano, na kuhakikisha matumizi sahihi ya fursa zitokanazo na Itifaki, mikataba na makubaliano ya kimataifa.

### 3.3.1. Lengo la Sera

Kuongeza tija katika matumizi ya mikataba, makubaliano na itifaki za kimataifa.

### 3.3.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuandaa utaratibu wa kusimamia na kuratibu mikataba, makubaliano, maazimio na itifaki;

ii. Kujenga uwezo unaohitajika ili kuhakikisha matumizi sahihi ya nyenzo za kisheria za kimataifa;

iii. Kubainisha maeneo ya kimkakati na maslahi ya Tanzania kimataifa; na

iv. Kuweka mikataba, makubaliano, maazimio na itifaki za kimataifa katika mfumo wa kisheria.

## 3.4. Ushirikiano wa Uwili

Tanzania inadumisha uhusiano ya uwili na nchi mbalimbali ili kukuza maslahi ya pande zote. Ushirikiano huu unatekelezwa kupitia tume za pamoja za ushirikiano, ziara za kidiplomasia, ushirikiano na miongozo mingine kwa maeneo mahsusi ya ushirikiano. Aidha, utekelezaji wa sera ya ujirani mwema unaendelea kuwa sehemu muhimu katika kukuza na kulinda uhusiano wa kihistoria, huku nchi zikitatua changamoto kwa pamoja kama vile uhalifu wa mipakani, uhamiaji haramu na maafa.

Tanzania itaendelea kukuza ujirani mwema pamoja na kushiriki katika ushirikiano wa uwili na nchi nyingine kama njia ya kubainisha na kutumia fursa za maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, Tanzania itahakikisha inaimarisha wigo na dhamira yake katika maeneo ya ushirikiano.

### 3.4.1. Lengo la Sera

Kuimarisha ushirikiano wa uwili

### 3.4.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kukuza na kudumisha ujirani mwema; na

ii. Kuimarisha na kupanua wigo wa uhusiano na ushirikiano wa uwili na nchi nyingine.

## 3.5. Mtangamano wa Kikanda

Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu, Jumuiya ya Nchi Zilizo Mwambao wa Bahari ya Hindi na Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA). Maeneo haya ya mtangamano wa kikanda yanatoa fursa muhimu kwa maendeleo ya biashara, kukuza ajira, kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa kuimarisha uratibu wa kanda na utafutaji wa mitaji ya uwekezaji. Maeneo mengine ni maendeleo ya viwanda, usimamizi wa fedha na bajeti, kuongeza kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuboresha miundombinu.

Hata hivyo, utekelezaji wa mtangamano wa kikanda unakumbwa na changamoto mbalimbali kama vile vikwazo vya biashara, miundombinu dhaifu, utekelezaji hafifu wa makubaliano katika mtangamano, sekta binafsi kutochangamkia ipasavyo fursa zilizomo na kukosekana kwa utoshelevu wa kibiashara kwa nchi wanachama. Kukabiliana na changamoto hizo kunahitaji jitihada za pamoja kikanda. Hivyo, Tanzania inasisitiza mtangamano wa kikanda kuhakikisha manufaa ya pamoja kupitia kukuza uchumi, programu za maendeleo za kikanda, kuongeza tija kwa sekta zote na kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu.

Vilevile, Tanzania inaunga mkono jitihada za kuimarisha usalama wa kikanda na kukuza amani na maendeleo endelevu. Hivyo, Tanzania itakuwa mstari wa mbele na kuchagiza makubaliano ya ushirikiano na utekelezaji wenye tija wa mikataba ya kikanda kama nyenzo muhimu ya kukuza maendeleo endelevu. Ili kufikia malengo hayo, Tanzania itaimarisha usimamizi, uratibu na utekelezaji wa ajenda za mtangamano wa kikanda.

### 3.5.1. Lengo la Sera

Kuongeza faida za mtangamano wa kikanda.

### 3.5.2 Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuunga mkono ajenda ya mtangamano wa Umoja wa Afrika na kuimarisha ushiriki wa wadau katika mtangamano wa kikanda;
ii. Kuweka mazingira wezeshi ya kuboresha ushindani na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda ; na
iii. Kuongoza jitihada za kufungamanisha makundi ya kikanda ya mtangamano wa kiuchumi.

## 3.6. Ushirikiano wa Kimataifa

Tanzania inaunga mkono kikamilifu jukumu la Umoja wa Mataifa katika kuimarisha amani na usalama wa kimataifa ili kukuza maendeleo endelevu. Mfumo wa Umoja wa Mataifa unahamasisha jitihada za pamoja kimataifa katika kukabiliana na changamoto za kiusalama na maendeleo. Hatua hii itafanikiwa kupitia uwepo wa ushirikiano wa pamoja. Kwa muktadha huo, kuendelea kukosekana kwa utulivu wa uchumi wa dunia, ongezeko la idadi ya watu, uhalifu wa kimataifa, uharibifu wa mazingira na ubaguzi katika nyanja mbalimbali vinaakisi umuhimu wa kuwa na juhudi za pamoja kimataifa ambazo Tanzania ni sehemu yake.

Kwa msingi huo, Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa na mashirika yake ili kupata suluhisho

la kudumu kwa changamoto zinazoikabili dunia. Aidha, Tanzania itaunga mkono mageuzi ya kitaasisi ili kuhakikisha dunia inafanya kazi kwa pamoja kukabiliana na changamoto mbalimbali. Hatua hii itawezesha Tanzania kunufaika zaidi na fursa za programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia mfumo wa Umoja wa Mataifa.

Vilevile, Tanzania itaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Madola, Ushirikiano wa Nchi Zinazoendelea na jumuiya nyingine za kimataifa kuhakikisha ushirikiano katika kuleta mageuzi ya mfumo wa ushirikiano wa kimataifa, na kuakisi mahitaji mahsusi ya nchi mbalimbali. Aidha, Tanzania itaendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje kupitia makubaliano ya kimataifa katika Shirika la Biashara Duniani – WTO na kuunga mkono uundaji wa mfumo wa kibiashara unaozingatia kanuni, unaotabirika, wenye uwazi na haki.

### 3.6.1. Malengo ya Sera

Kuhakikisha matumizi ya tija ya manufaa yanayotokana na Mfumo wa Umoja wa Mataifa na majukwaa ya kimataifa.

### 3.6.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa katika kudumisha amani na utatuzi wa migogoro duniani;
ii. Kuhakikisha programu na miradi ya kimataifa inayotekelezwa Tanzania inafungamana na vipaumbele vya maendeleo ya Taifa;
iii. Kuimarisha ushirikiano na taasisi za fedha za kimataifa;

iv. Kuunga mkono mageuzi ya kitaasisi ya Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa ili kuweka utaratibu wenye tija na unaoheshimu usawa na uhuru wa nchi; na

v. Kuimarisha ushirikiano na taasisi za kimataifa ikijumuisha Jumuiya ya Madola na Ushirikiano wa Nchi Zinazoendelea.

## 3.7. Kiswahili Kama Nyenzo ya Diplomasia

Kiswahili ni lugha maarufu inayozungumzwa na watu wengi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Kiswahili kinakuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, katika kukuza Kiswahili, UNESCO ilitangaza tarehe 7 Julai kila mwaka kuwa siku ya lugha ya Kiswahili duniani. Kiswahili kimetumika kama nyenzo ya mapambano ya uhuru, utambulisho wa Taifa, utu na lugha ya kuleta mshikamano kwa waafrika wote na watu wenye asili ya Afrika duniani hususan maeneo ya Marekani, Karibe na Ulaya.

Pamoja na kufanyika juhudi hizo, lugha ya Kiswahili haijaweza kutumika ipasavyo kuleta manufaa ya kiuchumi katika uhusiano wa kimataifa. Hii inatokana na Kiswahili kutotumiwa kama bidhaa, utangazaji mdogo na kutokuthaminisha bidhaa za Kiswahili. Aidha, kumekuwa na matumizi madogo ya Kiswahili kama lugha ya diplomasia katika taasisi za kikanda hususan katika vyombo vya maamuzi na vya kitaalamu.

Kwa msingi huo, kuna haja ya kuchukua hatua madhubuti za kutumia Kiswahili kwa manufaa ya kiuchumi katika uhusiano wa kimataifa na kuongeza matumizi yake kama lugha ya

kidiplomasia katika mijadala ya kikanda kwa ngazi zote. Aidha, Tanzania itaendelea kuweka jitihada za kuhakikisha Kiswahili kinajumuishwa katika fasihi, taaluma na sanaa na ubunifu, ikiwa ni pamoja na filamu na muziki ndani na nje ya nchi.

#### 3.7.1. Lengo la Sera

Kuwezesha matumizi ya Kiswahili kwa manufaa ya kiuchumi katika uhusiano wa kidiplomasia.

#### 3.7.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuwezesha matumizi ya Kiswahili kwa manufaa ya kiuchumi katika uhusiano wa kimataifa; na
ii. Kukuza matumizi ya Kiswahili kama lugha kuu barani Afrika na lugha ya kidiplomasia katika taasisi za kikanda na kimataifa.

## 3.8. Utafutaji wa Rasilimali

Utafutaji na utumiaji wa rasilimali za kimataifa unategemea maelewano na ushirikiano kati ya nchi na washirika wa maendeleo wa kimataifa, ukiungwa mkono na sera madhubuti. Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 unasisitiza kuangaliwa upya kwa mfumo wa kimataifa wa kifedha ili kufungua milango kwa nchi zinazoendelea kunufaika na vyanzo vya fedha kwa masharti nafuu. Kadhalika, Sera inasisitiza uwepo wa majadiliano ya pamoja kwa nchi zinazoendelea na zile zenye madeni ili kuwezesha kufutiwa madeni hayo.

Ili kufikia malengo hayo, Tanzania ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Deni

wa Muda wa Kati, Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Taifa, Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (2017/18 – 2024/25), Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani, utekelezaji wa Sheria ya Bajeti, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada.

Licha ya jitihada zilizofanyika, kutotabirika kwa mfumo wa kimataifa wa kifedha; kubadilika mara kwa mara kwa masharti ya kupata fedha na kubadilika kwa vipaumbele vya baadhi ya washirika wa maendeleo; ni vikwazo vinavyoendelea kufanya utafutaji na utumiaji wa rasilimali fedha kimataifa kuwa mgumu. Hali hii inaakisi umuhimu wa kujumuisha vyanzo vingine vya rasilimali kama vile mtaji watu na teknolojia katika kugharamia maendeleo ya Taifa.

Kwa muktadha huo, Sera ya Mambo ya Nje itawezesha utafutaji wa rasilimali kutoka nje utakaoendelea kutegemea vyanzo vya jadi wakati ikihamasisha vyanzo bunifu vya rasilimali zisizo za kifedha, kama rasilimali watu, uhawilishaji wa teknolojia, ushirikiano wa kimkakati na kuunga mkono ajenda ya maendeleo ya Taifa.

### 3.8.1. Lengo la Sera

Kuimarisha utafutaji wa rasilimali za kimataifa kwa maendeleo ya Taifa.

### 3.8.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuimarisha utafutaji wa rasilimali za kimataifa kwa vyanzo vya asili na vyanzo mbadala; na
ii. Kunufaika na rasilimali za kimataifa katika kuendeleza nguvu kazi, uhawilishaji wa teknolojia na ushirikiano kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

## 3.9. Uchumi wa Buluu

Uchumi wa Buluu unatoa fursa ya kuhifadhi vyanzo vya maji na kutumia kwa uendelevu rasilimali zilizopo. Kwa kuzingatia vyanzo vya maji vilivyopo nchini ni muhimu kutumia fursa zinazotokana na uchumi wa buluu ikijumuisha uvuvi, ufugaji wa viumbe vya baharini na usafirishaji wa bidhaa zitokanazo na bahari. Maeneo mengine ni miundombinu, nishati, umwagiliaji, uchimbaji wa madini, utalii na usimamizi wa shughuli za baharini. Kutokana na upana wake wa kipekee uchumi wa buluu unalenga kuleta maendeleo jumuishi, maendeleo ya jamii na uhifadhi wa mazingira kwa kuzingatia Sheria ya Ukanda Huru wa Uchumi wa Bahari ya Mwaka 1989 na Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya Mwaka 1998.

Kimataifa, dhana ya uchumi wa buluu inafungamanishwa na Lengo la 14 la Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya 2030 ya Maendeleo Endelevu; Lengo la 6 la Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063 "Afrika Tuitakayo"; Sheria ya Umoja wa Mataifa ya Mkataba wa Bahari na Azimio la Uchumi wa Buluu la Mwaka 2017 la Jumuiya ya Nchi Zilizo Mwambao wa Bahari ya Hindi. Ili kufungamanishwa na muundo wa usimamizi na kunufaika na fursa za uchumi wa buluu, Tanzania imeweka jitihada katika usimamizi wa vyanzo vya maji kwa kuanzisha Ukanda Huru wa Uchumi wa Bahari (EEZ) na kushirikiana na taasisi za kimataifa kusimamia shughuli za bahari kuu.

Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na changamoto za uchafuzi wa mazingira ya baharini unaovuka mipaka, athari za mabadiliko ya tabianchi, uharamia baharini, milipuko ya magonjwa, rasilimali zilizofungiwa katika sakafu ya bahari, na ukosefu wa mkakati wa pamoja wa uhifadhi. Kwa hali hiyo, Tanzania itaendelea kushirikiana na jumuiya ya kimataifa kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na vyanzo vyote vya maji.

#### 3.9.1. Lengo la Sera

Kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na vyanzo vingine vya maji.

#### 3.9.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa katika uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za baharini na vyanzo vyote vya maji nchini;
ii. Kuhakikisha uzingatiwaji wa sheria za kimataifa katika matumizi endelevu ya rasilimali za baharini na vyanzo vingine vya maji; na
iii. Kuhakikisha ulinzi na usalama wa bahari kwa kushirikiana na taasisi husika za kimataifa.

## 3.10. Ushirikishwaji na Ushiriki wa Diaspora

Diaspora ni washirika muhimu katika maendeleo ya kitaifa, ndiyo maana Serikali imeongeza jitihada kuwawezesha kuchangia kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Tanzania ina jumuiya ya diaspora muhimu katika nchi mbalimbali duniani. Hii imefanya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka utaratibu na mifumo ya usimamizi wa masuala ya diaspora, ambapo Wizara yenye dhamana ya mambo ya nje imekasimiwa jukumu hilo. Kwa Zanzibar suala la diaspora lipo chini ya Ofisi ya Rais. Serikali inatambua kuwa jumuiya za diaspora ambazo zimesajiliwa katika nchi wanazoishi ni sehemu ya wadau muhimu wa Serikali katika uhusiano wa kimataifa.

Pamoja na kuwa manufaa ya diaspora katika maendeleo ya Taifa yamebainishwa, bado fursa hiyo haijatumiwa ipasavyo. Hii inatokana na kutokuwepo kwa utaratibu mahsusi wa kuwezesha ushiriki wa diaspora na kukosekana kwa taarifa na takwimu sahihi zitakazosaidia Serikali kutambua mchango wa diaspora kwenye maendeleo ya Taifa. Aidha, kuna upungufu wa mwongozo wa sera na sheria wa kushirikisha diaspora ambao ni *Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania* kuchangia maendeleo ya Taifa lao la asili. Hivyo, ni muhimu kuweka taratibu rasmi za kushirikisha diaspora, hasa *Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania* katika kuunga mkono ajenda ya maendeleo ya Taifa na kwa kuzingatia asili yao. Hili litawezekana kwa kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria na upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi za mchango wa diaspora.

### 3.10.1. Lengo la Sera

Kuimarisha ushiriki wa diaspora katika maendeleo ya Taifa.

### 3.10.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuwezesha mahitaji ya diaspora ikiwa ni pamoja na kutoa Hadhi Maalum kwa Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania;

ii. Kuweka utaratibu rasmi wa ushirikishwaji wa diaspora katika ajenda ya maendeleo ya Taifa;

iii. Kuhakikisha Watanzania wananufaika na fursa za soko la ajira la kimataifa; na

iv. Kuhakikisha upatikanaji wa takwimu bora za diaspora.

## 3.11. Haki za Binadamu na Utawala Bora

Tanzania inazingatia na kuheshimu misingi ya haki za binadamu na utawala bora kwa kuhakikisha utu na haki nyingine za binadamu zinaheshimiwa na kuenziwa. Ahadi hizi zimeainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sehemu ya Tatu kuhusu Haki na Wajibu wa Msingi hususan Ibara ya 29 (1) inayotamka kuwa "Kila mtu katika Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu, na matokeo ya kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii."

Vilevile, Tanzania inazingatia haki za binadamu kwa mujibu wa mikataba na itifaki za kimataifa za haki za kiraia na kisiasa. Kwa muktadha huo, Tanzania imesaini nyenzo za kikanda na kimataifa ikijumuisha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1945 na kuridhia Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) wa mwaka 1948; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Vienna kuhusu Sheria ya Mikataba wa mwaka 1969. Vilevile, Tanzania imesaini Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981, na Mkataba wa SADC wa Haki Muhimu za Kijamii wa mwaka 2003.

Katika kutekeleza suala hili, Tanzania ina utaratibu wa kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu masuala ya haki za binadamu. Taratibu hizi zinajumuisha sheria kama vile Sheria ya Haki na Wajibu Muhimu ya mwaka 1994, Sheria ya Utajiri na Rasilimali za Nchi ya Mwaka 2017 na uanzishwaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Idara huru ya Serikali ya kukuza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Aidha, Tanzania inatoa fursa kwa wadau walio nje ya Serikali kama vile vyombo vya habari, asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu masuala ya haki za binadamu nchini. Kukuza na kulinda haki za binadamu, utawala bora

na demokrasia hutoa fursa kwa Tanzania kushiriki kikamilifu katika mahusiano wa uwili, kikanda na kimataifa kwa kuzingatia tunu na msingi ya kijamii na kiutamaduni.

#### 3.11.1. Lengo la Sera

Kusimamia haki za binadamu na utawala bora kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kuzingatia mila na desturi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

#### 3.11.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kukuza haki za binadamu kwa kuzingatia mila, desturi, maadili na tamaduni za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na
ii. Kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika masuala yote yanayohusu haki za binadamu.

### 3.12. Masuala Mtambuka

#### 3.12.1. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi yameathiri takribani sekta zote Tanzania ikiwemo ukame, upepo mkali, kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu, mabadiliko ya misimu ya mvua na mafuriko. Hali hii inasababisha uhaba wa maji, kupungua kwa usalama wa chakula, kuongezeka kwa jangwa na mabadiliko ya mfumo wa ikolojia. Aidha, ongezeko la kina cha maji kutokana na

mabadiliko ya tabianchi limesababisha kuzama kwa baadhi ya visiwa na kuingia kwa maji ya bahari katika visima pamoja na uharibifu wa shughuli nyingine kwenye fukwe za bahari.

Tanzania imechukua hatua za kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na, kutekeleza programu ya Kudhibiti Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (2011), kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026), kuridhia na kuanza kutekeleza Itifaki ya Kyoto (2002), Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Paris (2018) na Mpango wa Mchango wa Taifa wa Kupunguza Gesi Chafuzi (2021), kuandaa Sera ya Taifa ya Mazingira (2021) na kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Kanuni na Mwongozo wa Kitaifa wa Biashara ya Hewa Ukaa (2022).

Licha ya jitihada hizo, changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi zimeendelea kuwepo, hivyo juhudi zaidi zinahitajika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, jitihada hizo zinakumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upatikanaji mdogo wa fedha na teknolojia  kutoka katika na mifuko ya kimataifa ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, Sera ya Mambo ya Nje itawezesha kuimarisha ushirikiano na mashirika ya kimataifa katika usimamizi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

#### 3.12.1.1. Lengo la Sera

Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

#### 3.12.1.2. Matamko ya Sera

Serikali itawajibika:

i. Kuhakikisha ushiriki wenye tija wa Tanzania katika majadiliano ya kimataifa kuhusu usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na
ii. Kuhakikisha upatikanaji na utumiaji sahihi wa rasilimali fedha za nje katika usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### 3.12.2. Jinsia na Vijana

Kujumuishwa kwa masuala ya jinsia na vijana kwenye Sera kunatoa fursa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ni muhimu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka sera stahiki na kuchukua hatua katika uga wa kimataifa kutatua changamoto zinazowakabili vijana na wanawake. Hatua hii inaongeza nguvu jitihada za kitaifa kwa kuonesha umuhimu wa masuala ya usawa wa jinsia na fursa kwa vijana katika ushirikiano wa kidiplomasia na uhusiano wa kimataifa.

#### 3.12.2.1. Lengo la Sera

Kuhakikisha ujumuishwaji wa masuala ya usawa wa jinsia na fursa kwa vijana katika ushirikiano wa kimataifa.

#### 3.12.2.2. Tamko la Sera

Serikali itahakikisha ushiriki wenye tija wa vijana na wanawake katika masuala ya kimataifa.

# SURA YA NNE

# MUUNDO WA KISHERIA

# 4.0. Muundo wa Kisheria

Sura hii inaeleza muundo wa kisheria wa kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya 2001, Toleo la Mwaka 2024 katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa. Sera hii itatekelezwa kupitia sheria mbalimbali za nchi na nyenzo za kisheria za kimataifa ambazo zimeridhiwa na Tanzania.

Miongoni mwa vyombo vya kimataifa vitakavyosaidia utekelezaji wa Sera hii ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1945; Mkataba wa Vienna wa mwaka 1961 Unaohusu Uhusiano wa Kidiplomasia; Mkataba wa Vienna wa mwaka 1963 Unaohusu Uhusiano ya Kikonseli; Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Mwaka 2000; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 na itifaki zake; na Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992 na itifaki zake; na mikataba, itifaki, na makubaliano mengine ya uwili, kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Ufanisi katika utekelezaji wa Sera utahusisha mapitio, uwianishaji na maboresho ya sheria husika ikiwemo Sheria ya Uhamiaji, SURA 54, Sheria ya Ardhi, SURA 113; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu SURA 146 na Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu SURA, 388. Sekta husika zinatarajiwa kufanya mapitio ya sheria hizo kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa.

# SURA YA TANO

# MUUNDO WA KITAASISI

## 5.0. Muundo wa Kitaasisi

Ufanisi katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya 2001, Toleo la 2024 utahusisha wadau mbalimbali. Sera itatekelezwa kupitia Wizara, Idara na Taasisi kwa kujumuisha matamko ya Sera na Mikakati yake katika Mamlaka zao husika. Aidha, taasisi zisizo za Serikali zitakuwa muhimu katika kuwezesha utekelezaji wa Sera kwa kuwafikia wadau wengi hususan wananchi. Hivyo, ufanisi wa utekelezaji utategemea ushirikiano wa wadau katika ngazi ya Taifa, kanda na kimataifa. Majukumu ya kila mdau ni kama ifuatavyo:

**Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje** itakuwa mratibu na msimamizi wa mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Sera. Wizara itaunganisha wadau wote wa ndani na nje ya nchi katika kipindi chote cha utekelezaji wa Sera.

**Wizara yenye dhamana ya Ulinzi** itawezesha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika misheni za ulinzi wa amani nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kuwezesha utekelezaji wa Sera katika masuala ya amani, ulinzi na utulivu wa kisiasa katika ngazi za uwili, kikanda na kimataifa.

**Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi** itawezesha uratibu wa masuala yanayohusu uhamiaji; uingiaji na utokaji huru wa watu; ujirani mwema; programu za kukabiliana na uhalifu wa kimataifa na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Wizara zinazohusika na sekta za uchumi, huduma na uzalishaji kwa pande zote mbili za Muungano** zitajielekeza katika kuhakikisha Tanzania inakuwa mstari wa mbele kwenye utekelezaji wa diplomasia ya uchumi hususan biashara, utamaduni, utalii, utafutaji rasilimali, ukuzaji wa vipaji na kuvutia uwekezaji kwa fursa zilizopo.

**Wizara zenye dhamana ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa** zitawajibika kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sera yanayofungamana na mikoa na halmashauri katika maeneo ya kuwezesha uwekezaji, kilimo, maendeleo ya viwanda na biashara mipakani.

**Ofisi za Wanasheria Wakuu wa Serikal**i zitawajibika kutoa miongozo ya kisheria katika usimamizi wa nyenzo za kisheria za kimataifa.

**Wizara, Idara na Wakala Nyingine** zitahusika na utekelezaji wa Sera kwa kujumuisha majukumu yaliyoainishwa katika sera hii na sera za sekta husika, mikakati, mipango na programu zao.

**Sekta binafsi** itawajibika katika kukuza biashara, kutangaza utalii na kufanya uwekezaji. Aidha, sekta hii itasaidia kutoa mchango katika maeneo ya kuboresha pamoja na mrejesho kwa Serikali katika maeneo mahsusi kulingana na maslahi ya nchi.

**Taasisi za taaluma na tafiti** zitawajibika kufanya utafiti kuhusu masuala yanayohusiana na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje hususan diplomasia ya uchumi na kutumia matokeo ya tafiti hizo kwa ajili ya maamuzi yenye tija.

**Diaspora** watawajibika kuishauri Serikali na kuunga mkono jitihada za Tanzania za kijamii na kiuchumi hususan uwekezaji, utamaduni, biashara na utalii katika nchi wanazokaa. Aidha, diaspora watawezesha kubadilishana maarifa, ujuzi na teknolojia.

**Vyombo vya habari** vitasaidia programu za uhamasishaji, kujenga uelewa na kusambaza taarifa na elimu kwa umma kuhusu sera na masuala ya mambo ya nje nchini na nje ya nchi kwa ufanisi.

**Washirika wa Maendeleo** wataunga mkono juhudi za kitaifa katika ajenda ya maendeleo ikijumuisha upatikanaji wa rasilimali, ukuzaji wa ujuzi na uhawilishaji wa teknolojia.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia na Asasi za Kijamii** yataendeleza agenda ya sera ya mambo ya nje kwa kuwasilisha maudhui kwa wananchi, kutoa elimu na uhamasishaji wa umma, kuwezesha wananchi na kujenga mtandao wa kijamii kuhusu masuala ya mambo ya nje.

## 5.1. Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera ni sehemu muhimu katika utekelezaji malengo husika. Zoezi hili litahusisha upimaji wa viashiria vya utendaji wa kila lengo la sera. Aidha, utekelezaji wa sera utafuatiliwa na kufanyiwa tathmini katika kipindi chote cha utekelezaji kwa ngazi zote. Wizara yenye dhamana na mambo ya nje itaratibu wizara, idara na wakala wa Serikali na wadau muhimu katika ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji na kutoa taarifa kwa wakati katika mamlaka husika.

Vilevile, Wizara itafanya tathmini kila mwaka pamoja na tafiti kuhusu utekelezaji wa sera. Hatua hiyo itafuatiwa na kuandaa taarifa za utekelezaji na kuonesha matokeo kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo, tathmini ya jumla ya utekelezaji itafanyika baada ya miaka mitano.

## 5.2. Hitimisho

Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 ilifafanua maudhui, utaratibu na malengo ya Tanzania kushiriki katika uhusiano wa kimataifa. Msingi wa masuala ya mambo ya nje ulijumuisha kutokufungamana na upande wowote, Umoja wa Afrika, uhuru, usawa, maslahi ya Taifa na haki za binadamu. Aidha, Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mantiki ya kisiasa ya kujitawala kwa mataifa ya Afrika, na iliongoza harakati za ukombozi wa mataifa yote ya Afrika, ukombozi wa watu waliodhulumiwa, na kuendeleza Umoja wa Afrika. Hivyo, Sera ya Mambo ya Nje ililenga ukombozi, mshikamano na umoja wa nchi za Afrika.

Katika kipindi cha 2001 - 2023, Tanzania ilipata mafanikio katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kwa kuimarisha uhusiano wa uwili, ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Hii ilisababisha uchumi kukua kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka kutokana na kuongezeka kwa tija katika uzalishaji, kukua kwa biashara na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Mafanikio mengine ni uzalishaji wa ajira, ustawi wa jamii, maendeleo ya watu na kuongezeka kwa amani na usalama Afrika na sehemu nyingine duniani.

Licha ya mafanikio hayo, changamoto mbalimbali zimeendelea kuwepo katika masuala ya mambo ya nje ikiwemo uhalifu wa kuvuka mipaka na kimataifa, kukosekana kwa utulivu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa na utekelezaji hafifu wa nyenzo za kisheria za kimataifa zilizoridhiwa. Aidha, sera haikutoa mwelekeo wa ushiriki wa diaspora katika maendeleo ya taifa, matumizi ya Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia na matumizi ya rasilimali za baharini na vyanzo vingine vya maji katika kuendeleza uchumi wa buluu.

Sera ya Mambo ya Nje ya 2001 Toleo la Mwaka 2024 inalenga kufungamanisha ngazi zote za maendeleo, kitaifa, kikanda na kimataifa. Sera itaendelea kuweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi, kukuza amani, usalama na utulivu wa kisiasa, kuongeza tija katika matumizi ya mikataba, makubaliano, maazimio na itifaki za kimataifa, kuimarisha uhusiano wa uwili na kuongeza tija katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Vilevile, sera inakusudia kutumia Kiswahili katika uhusiano wa kimataifa, kutafuta rasilimali kwa maendeleo ya taifa, kutumia fursa za uchumi wa buluu kwa tija, ushiriki wa diaspora katika maendeleo ya taifa; kulinda haki za binadamu na utawala bora kwa misingi ya jamii na tamaduni za Tanzania; kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kujumuisha masuala ya jinsia na vijana katika ushirikiano wa kimataifa.

**Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,**
Mji wa Serikali- Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA.

Mawasiliano
Simu: +255-26- 2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208

Baruapepe: nje@nje.go.tz

mfa_Tanzania

foreign.go.tz